



BIMA YA AFYA KWA WANAFUNZI

- VYUO
- SHULE ZA SEKONDARI
- SHULE ZA MSINGI
- SHULE ZA AWALI

Uhakika wa Matibabu kwa Wote

TOLEO LA MEI 2021

www.nhif.or.tz

[Piga 199 bure](tel:199)

[f](#) [t](#) [@](#) nhiftz

[▶](#) NHIF ONLINE TV

BIMA YA AFYA KWA WANAFUNZI

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unatoa bima ya afya kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu, kati na ufundi, shule za sekondari, msingi na awali nchini kwa lengo la kuwawezesha kupata huduma za matibabu kwa gharama nafuu.

Mwanafunzi aliyesajiliwa atapata huduma za matibabu kupitia kadi yake ya bima ya afya wakati wote anapokuwa masomoni na wakati wa likizo. Huduma hizo zinapatikana katika vituo vya matibabu zaidi ya 9,000 vilivyosajiliwa na NHIF nchi nzima.

MAMBO YA KUZINGATIA

- Wanafunzi wote watajiandikisha chini ya udhamini wa shule, chuo au taasisi husika ya elimu.
- Kila mwanafunzi atalipia mchango wa Tsh. 50,400/= kwa mwaka.
- Mwanafunzi atahuisha uanachama wake kila mwaka kwa kuchangia kiasi hicho hicho hadi atakapohitimu masomo yake.

Mpango huu pia unaweza kutumika kwa watoto wa wanachama wa Mfuko waliozidi umri wa utegemezi ikiwa bado wako masomoni.

NAMNA YA KUJISAJILI

Ili kujisajili mwanafunzi atahitajika kufuata utaratibu ufuatao :-

- Shule/chuo/taasisi husika kujisajili kwenye Mfuko.
- Mwanafunzi wa shule/chuo/taasisi iliyosajiliwa na Mfuko ataweza kukamilisha usajili wake sambamba na kukamilisha usajili/udahili katika chuo/shule/taasisi kwa mwaka wa masomo husika.
- Mwanafunzi anapojiunga na chuo/shule/taasisi awasiliane na Mshauri wa wanafunzi kwa hatua za kujisajili na bima ya afya.

UKOMO WA UANACHAMA

Ukomo wa uanachama unasababishwa na:-

- Kuacha au kuachishwa masomo;
- Kuhitimu masomo;
- Kusitishwa kwa michango; na
- Kifo.

Huduma kwa Wateja Piga Simu bila Malipo

199